



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**  
**SHIRIKA LA TAIFA LA MAENDELEO**



**TAARIFA KWA UMMA**

**BAJETI WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA KUJIKITA KATIKA KUENDELEZA  
MIRADI YA KIMKAKATI YA LIGANGA NA MCHUCHUMA PAMOJA NA MRADI WA  
MAGADI SODA WA ENGARUKA**

Waziri wa viwanda na Biashara Mh. Dkt. Ashatu Kijaji amebainisha nia ya serikali ya kuhakikisha inaendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya Liganga na Mchuchuma pamoja na mradi wa Magadi soda wa Engaruka kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Haya yamebainishwa hii leo bungeni mjini Dodoma wakati Waziri huyo akiwasilisha bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo takribani kiasi cha shilingi bilioni 110,899,722,000 zimeidhinishwa na Bunge.

Akizungumza kuhusiana na ulipaji fidia katika utekelezaji wa mradi wa Magadi Soda uliopo Engaruka mkoani Arusha Mh. Waziri amesema Wizara kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imekamilisha maandalizi yote ya kuanza utekelezaji wa mradi wa Magadi Soda Engaruka ikiwa ni pamoja na kukamilisha upembuzi yakinifu, kupata cheti cha mazingira, utafiti wa kina wa kiwango cha rasilimali madini, uainishwaji wa miundombinu wezeshi, stadi ya masoko ya ndani na nje ya nchi, na uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Wizara ya Ardhi, na Halmashauri ya Monduli imekamilisha uhakiki wa fidia ambapo kiasi cha shilingi bilioni 14.5 kinatarajiwa kulipwa kwa wananchi 599 kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 60,884

Waziri pia amebainisha kuwa, Wizara imekamilisha zoezi la kugawanya eneo la mradi katika maeneo matatu (3) ambayo yatatangazwa kwa ajili ya kupata wawekezaji. Lengo kuu la kugawa eneo hilo ni kuwezesha kupata wawekezaji tofauti kwa kila eneo wenye uwezo wa kifedha, uzoefu na Masoko ambapo hadi sasa jumla ya wawekezaji 22 wameonesha nia ya kuwekeza kwenye eneo hilo.

Katika hatua nyingine Waziri pia amebainisha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi wa Liganga na Mchuchuma ambapo amebainisha kuwa Wizara chini ya uratibu wa

**Development House, Ohio Street/ Kivukoni, 6<sup>th</sup>Floor, P.O.BOX 2669, Dar es Salaam, TANZANIA**

Tel : (+255 - 22) 2111460/1, 2111463/4, Fax: (+255 – 22) 2113618, Email: [info@ndc.go.tz](mailto:info@ndc.go.tz), [ndc@ndc.go.tz](mailto:ndc@ndc.go.tz)  
Website: <http://www.ndc.go.tz>

Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imeendelea na ukamilishaji wa ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha Mradi huo. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya shilingi bilioni 15.414 zimelipwa kati ya shilingi bilioni 15.424 kwa wafidiwa 1,129 kati ya 1,142. Idadi ya wafidiwa waliolipwa ni sawa na asilimia 99.

Kuhusiana na idadi ya watu ambao hawajalipwa Mh. Waziri amesema kuwa kiasi ambacho hakijalipwa kwa Wafidiwa 13 ni milioni 10.227. Wananchi hao 13 hawajalipwa kwa sababu mbalimbali zikiwemo baadhi yao kutojitokeza, na wengine kutokamilisha nyaraka na taratibu za mirathi. Aidha ameongeza kuwa Juhudi za kuwapata wafidiwa hao au warithi wao zinaendelea kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Njombe na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ili zoezi lihitimishwe.

Mh. Waziri ameendelea kusema kuwa baada ya kuhitimisha zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi katika eneo la Mradi wa Liganga na Mchuchuma, Serikali inakamilisha taratibu za utwaaji wa Ardhi kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya kundeleza mradi huo ambapo kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na mwekezaji kwa nia ya kuhitimisha na kuanza utekelezaji wa mradi huo.

Katika hatua nyingine Mh. Waziri ameongeza kuwa Katika kuhakikisha nchi inanufaika na rasilimali kubwa ya makaa ya mawe yaliyopo Mkoa wa Njombe, Wizara ilisaini mikataba na wachimbaji wadogo (Primary Mining Licences) wa Makaa ya Mawe kwenye eneo la vitalu 10 lilitopo nje ya mkataba wa mradi wa Mchuchuma na Liganga mnamo mwezi Septemba, 2023. Aidha, maandalizi ya awali ya utafiti na uchimbaji kwenye leseni ndogo 23 yameanza ambapo kampuni mbili (2) zimekamilisha taarifa ya kijiolojia na kampuni nyingine zinaendelea na utafiti wa kijiolojia. Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha miradi hiyo inaanza uzalishaji mapema.

Imetolewa na Kitengo ya Mawasiliano na Masoko,

Shirika la Taifa la Maendelo (NDC),

Dodoma

Mei 21, 2024